

**Taswira za Wanyama katika Mashairi ya Kezilahabi**Wael Nabil Ibrahim Othman<sup>1</sup>

Chuo Kikuu cha Al-Azhar

**Ikisiri**

Kezilahabi ni mhakiki na mtunzi maarufu wa ushairi, riwaya na tamthilia. Katika ushairi, ameandika diwani tatu ambazo ni *Kichomi* (1974), *Karibu ndani* (1988), na *Dhifa* (2008). Aidha, wahakiki wengi waliobobeaa katika fasihi ya Kiswahili wanaafikiana kwamba Kezilahabi ametumia kipengele cha taswira au picha katika kazi zake za kifasihi hasa katika mashairi yake kwa ufundi mkubwa. Miongoni mwao ni Senkoro (1988) anasisitiza kwamba ufundi wa taswira umezagaa katika diwani ya *Kichomi* iliyoandikwa na Kezilahabi, na kwamba shairi ambalo limetajwa na wahakiki wengi kuwa ni maarufu na ni kielelezo cha ufundi wa Kezilahabi katika matumizi ya taswira ni lile la “Nimechoka”. Kadhalika, Saleh (1990) anafafanua kuwa picha ni kipengele muhimu sana katika mashairi ya Kezilahabi. Wamitila (1998) pia anaeleza kwamba Kezilahabi ni mwandishi ambaye yupo katika ngazi ya juu ya waandishi wanaomakinikia ujenzi tata wa ishara na taswira katika fasihi ya Kiswahili, kiasi kwamba ni vigumu kwa msomaji wa juujuu kufanikiwa kuziibua na kuzitafakari kwa kina mbinu zake. Kwa ujumla, maoni ya wahakiki waliowahi kuzichunguza kazi za Kezilahabi yanathibitisha kuwa kazi mbalimbali za kishairi zilizoandikwa na Kezilahabi zimesheheni matumizi makubwa ya taswira. Pamoja na mambo mengine, makala haya yanaendeleza mijadala wa matumizi ya taswira katika kazi za mtunzi huyu hasa kwa kuangazia dhana ya taswira, dhamira zinazoendelezwa na mtunzi kwa kutumia taswira husika pamoja na makundi au kategoria za taswira zijengwazo kwa kutumia wanyama.

**1.0 Utangulizi**

Suala la matumizi ya taswira katika kazi za kifasihi limejadiliwa na wataalamu wengi. Wataalamu hao wametoa maoni na maelekezo ambayo ni mwafaka katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Mathalani, wameelezea dhana ya taswira, aina za taswira na dhima yake katika kazi hizo. Miongoni mwa waliofanua dhana ya taswira ni Mbatia (2001:25). Mtaalamu huyu

---

<sup>1</sup> Baruapepe: Wael\_Nabil@Azhar.edu.eg

anabainisha kwamba taswira ni kunga ya utunzi ambapo lugha inatumiwa kusawiri picha fulani. Taswira au picha hizo hujengwa kwa kutumia lugha au maneno teule yaliyosheheni tamathali mbalimbali za usemi. Kwa upande wake Wamitila (2003:225), anafafanua kwamba dhana ya taswira hutumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Mtaalamu huyu anaongeza kuwa istilahi ya taswira na jazanda zinahusiana kwa kiasi kikubwa. Vilevile, Wamitila (2004:197) anasisitiza kuwa taswira ni neno linalotokana na lugha ya Kiarabu na linatumika au kumaanisha sawa na neno ‘jazanda’ lenye asili ya lugha ya Kibantu.

Maoni ya Wamitila (2004) kwamba jazanda na taswira zinahusiana pia yamewahi kutolewa na Mazrui (1992) ambaye aeleza kuwa hakuna tofauti kati ya taswira na jazanda. Kwa ufupi, Mazrui (1992: 38) anafafanua kuwa taswira au jazanda ni ule ubingwa wa lugha unaotumiwa na mtunzi katika kusimulia au kuchora picha ya kitu kikaonekana dhahiri kabisa; yaani usimulizi wenyewe kunasa nadhari na hisia za msomaji. Naye Msokile (1993: 45) anapozungumzia taswira anaeleza kuwa taswira ni neno lenye matumizi mbalimbali katika uhakiki wa fasihi. Msokile (1993: 83) anaongezea kwa kusema kuwa jazanda ni lugha ya kipicha, lugha ya kitaswira (*imagery*). Ni lugha ambayo huchora picha ya suala linalojadiliwa kisanaa kwa kutumia tamathali za usemi. Maelezo ya Msokile pia yanashabihiana na maelezo yaliyotolewa na Njogu na Chimerah (1999: 33) waliobainisha kwamba taswira ni mkusanyiko wa picha anazozipata msomaji au msikilizaji baada ya kusoma, kuona, au kusikiliza kazi ya fasihi kwa minajili ya kutoa funzo fulani. Jambo hili pia limesisitizwa na Madumulla (2009: 150-153) hasa pale aliposema kuwa si rahisi sana kutenganisha baina ya picha/taswira, ishara na jazanda.

Kwa ujumla, kutokana na maelezo yaliyotolewa na wataalamu mbalimbali, tunabaini kwamba taswira ni picha moja au mkusanyiko wa picha mbalimbali anazopata msomaji au msikilizaji kupitia kazi ya fasihi. Taswira ni mbinu ya kisanaa hususan matumizi ya lugha inayotumiwa na mtunzi ili kusawiri picha fulani akilini mwa msomaji au msikilizaji. Hii ina maana kuwa taswira ni mojawapo ya mbinu za sanaa zinazohusiana na matumizi ya lugha katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Kupitia mbinu hii mtunzi anaweza kueleza mawazo maalumu yaliyomo ndani yake.

Licha ya hivyo, maoni ya wataalamu yaliyorejelewa hivi punde yanasisitiza umuhimu wa tamathali za usemi hasa tashbihi au tashbiha, na istiara katika kujenga taswira za namna mbalimbali. Imeelezwa kuwa tashbihi au tashbiha

ambazo ni maelezo yanayolinganisha na kuhusisha vitu vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile (Madumulla, 2009: 147) husaidia kujengea taswira kwa njia ya kulinganisha na kulinganua. Aidha, taswira hutumia isitiara, ambayo ni mbinu ya kuielezea hali ambapo hadithi fulani inaweza kufasiriwa au kusomwa kwa namna tofautitofauti (Wamitila, 2003: 69). Vilevile, taswira hutumia ishara ambayo ina maana ya alama au dalili kama alivyotaja Msokile (1993: 82). Hata hivyo, jazanda hutumiwa hasa kuelezea sifa za matumizi ya picha au taswira kwa ujumla wake. Tunaposema kuwa kazi fulani ina jazanda, tunalenga kwenye ujumla wa matumizi ya taswira ambazo zinaweza kuwa za aina mbalimbali. Kwa ujumla, taswira ni mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya msanii katika kazi ya fasihi. Katika fasihi, taswira hujengwa kutokana na matumizi ya tamathali za usemi, hasa za sitiari na tashbiha mbalimbali zenyenye kuhusu mawazo, dhana vitu, na umbile.

Kadhalika, ujenzi wa taswira hutumika kimkakati kwa minajili ya kuwasilishia fikra za msanii kwa hadhira. Kwa hivyo, maelezo ya wataalamu hawa yanatuambia kuwa matumizi ya taswira humfanya msomaji au hadhira ipate aina mbalimbali za hisi zinazoshughulikiwa na kazi mahususi ya kifasihi; yaani hisi za kunusa, kuona, kugusa, kuonja na kusikia. Aidha, kama alivyowahi kupendekeza Senkoro (2011:30) kuna matumizi mbalimbali ya taswira katika uhakiki wa fasihi, na kila mtunzi hutumia taswira hizo kwa madhumuni mahususi.

Aina hizi za taswira zinazorejelewa na wataalamu mbalimbali pia tunaziona zikitajwa mara kwa mara kwenye marejeleo mbalimbali. Mathalani, Wamitila (2003: 225-227) ameainisha makundi kadhaa ya taswira. Makundi hayo ni pamoja na taswira kuu, za msingi, za harufu/mnuso, kimaelezo, kiishara, joto, mguso, mwendo, vionjo na ubaguzi/utenganishaji.

Taswira kuu hurejelea aina za taswira ambazo zinatumika kuelezea taswira au sitiari inayotawala au kuchukua nafasi kuu katika maudhui ya kazi ya fasihi. Hizi ni tofauti na taswira za msingi ambazo huchukua nafasi kubwa katika muundo wa kazi ya fasihi badala ya maudhui. Taswira za harufu/mnuso ni zile ambazo humletea msomaji picha zinazohusiana na harufu. Taswira za kimaelezo ni zile ambazo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au lugha anayoitumia. Pia, taswira za kiishara ni taswira ambazo hufanya kazi kama ishara. Vilevile, taswira za joto huhusiana na joto na taswira za mguso ni zile ambazo hujenga picha ya kitu thabiti au kitu kinachoweza kugusika. Halikadhalika, taswira za mwendo ni zile zinazomletea msomaji picha za mwendo na taswira za vionjo hulenga kwenye hisia ya kuonja ilhali katika

taswira za usikivu msanii anaunda pitcha ambazo hulenga hisia ya kusikia. Hatimaye, taswira za ubaguzi au utenganishaji ni kundi la taswira zinazoelezea pitcha ambazo zinatumwiwa kama msingi wa kulitenga au kulibagua kundi fulani la wanajamii au watu.

## **2.0 Diwani za Kezilahabi Zilizochunguzwa**

Makala haya yamerejelea kazi tatu za Kezilahabi ambazo ni *Kichomi*, *Dhifa* na *Karibu Ndani*. Diwani ya *Kichomi* ina mashairi arobaini na mawili. Mtunzi ameyagawanya mashairi yaliyomo kwenye diwani yake katika makundi mawili. Kundi la kwanza linaitwa *Mashairi ya Mwanzo*. Inaelezwa kuwa kwa mara ya kwanza mashairi haya yalitungwa kwa lugha ya Kiingereza, baadaye yakatafsiriwa kwa Kiswahili. Kundi la pili linaitwa *Fungueni Mlango*. Kundi hili limegusia maana ya maisha.

Aidha, diwani ya *Karibu Ndani* ina mashairi ishirini na mawili. Kwa mujibu wa yaliyotajwa kwenye jalada la nje la diwani hii (Kezilahabi, 1988), mashairi haya ni kiwakilishi kamili cha mawazo yaliyomshughulisha mtunzi katika diwani yake ya kwanza (*Kichomi*).

Kwa upande mwingine, diwani ya *Dhifa* ina mashairi hamsini na mawili. Katika utangulizi wa diwani hii, Wamitila (2008) anaelezea nafasi na umuhimu wa mtunzi wa diwani hii katika historia ya fasihi ya Kiswahili, na umahiri wake katika kutumia lugha ya kawaida iliyosheheni mazungumzo na inayotumika kila siku. Wamitila anataja masuala yaliyojadiliwa katika diwani hii kuwa ni pamoja na utawala, ubaguzi, maana ya maisha na tafakuri nyinginezo za kifalsafa kama vile hali ya kuwako kwa binadamu ulimwenguni, kifo, na safari. Vilevile, mwandishi wa utangulizi wa diwani hii amefafanua kuwa ucheshi na taswira ni mionganoni mwa sifa muhimu za kifani zilizotumiwa katika diwani hii.

## **3.0 Kezilahabi na Watunzi wengine Waliomtangulia**

Kwa kuzingatia kigezo cha matumizi ya taswira, ujumi wa kishairi unaojitokeza katika kazi za Kezilahabi unaweza kulinganishwa na ule unaojitokeza katika kazi za Mnyampala. Katika *Diwani ya Mnyampala*, Mnyampala ametumia taswira na amezigawa katika mafungu makuu matatu (Senkoro, 2011: 31-33): taswira zionekanazo, taswira za mawazo, na taswira za hisi. Aidha, kazi za Kezilahabi zinaelekeana na kazi za Shaaban Robert. Kwa mujibu wa Senkoro (2011: 34-35) ushairi wa Shaaban Robert umetumia taswira za aina mbalimbali kama vile taswira za maumbile (hali ya hewa angani, hali ya hewa juu ya ardhi, hali ya hewa chini ya ardhi); taswira za viumbe (watu, wanyama, wadudu, na kadhalika); taswira za viumbe wasio na

mwili (majini, mashetani, na kadhalika). Kwa hivyo, inaonekana kuwa Kezilahabi ameathirika sana na washairi Waswahili waliomtangulia hasa Shaaban Robert na Mathias Mnyampala katika suala la taswira.

#### **4.0 Taswira za Wanyama katika Mashairi ya Kezilahabi**

Matumizi ya taswira katika mashairi ya Kezilahabi yamegawanyika katika mafungu matatu: taswira za maumbile, taswira za viumbe wasio na mwili, na taswira za viumbe. Msomaji wa mashairi ya Kezilahabi anaweza kuangalia fungu la kwanza (taswira za maumbile) kuitia mashairi kama vile: “Upepo wa Wakati” (Kezilahabi, 1974: 4), “Kilio Kijijini” (Kezilahabi, 1988: 17), na “Bonde” (Kezilahabi, 2008: 29), ... n.k. Pia, anaweza kuangalia fungu la pili (taswira za viumbe wasio na mwili) kuitia mashairi kama vile: *Mganga* (Kezilahabi, 1974: 10), *Sisi kwa Sisi* (Kezilahabi, 1988: 19-20), na *Zimwi* (Kezilahabi, 2008: 40), ... n.k. Vilevile, anaweza kuangalia fungu la tatu (taswira za viumbe) kuitia mashairi kama vile: *Uvuaji wa Samaki Victoria* (Kezilahabi, 1974: 9), *Kujifunza Kuendesha* (Kezilahabi, 1988: 29), na *Kwa Walimu Wote* (Kezilahabi, 2008:1-2), ... n.k.

Aidha, ni dhahiri kwamba mionganoni mwa viumbe ambao Kezilahabi amewatumia kujengea taswira mbalimbali ni wanyama. Baadhi ya wanyama hawa ni wa nyumbani, wapo pia wa porini, na wengine ni wa baharini. Hata hivyo, taswira hizi za wanyama hazitumiwi kiholela. Kila taswira inabeba maana au ujumbe maalumu ambao umekubaliwa na jamii ya Waswahili. Bila shaka kuitia kila taswira na ujumbe wake, mtunzi amekusudia kugusia dhamira maalumu. Katika sehemu ifuatayo tumetalii kwa umahususi masuala yanayogusisha na mshairi huyu kuitia taswira za wanyama anazotumia.

#### **4.1 Dhamira ya Ukoloni**

Ukoloni ni mfumo wa kiutawala ambapo taifa moja lisilo na nguvu hutawaliwa na taifa jingine lenye nguvu zaidi (Bakhressa, 1992: 419). Kezilahabi amegusia dhamira ya ukoloni katika mashairi yake huku akitumia taswira za viumbe wa baharini kama vile samaki, na wanyama wa porini kama vile fisi.

##### **4.1.1 Samaki**

Samaki ni kiumbe anayeishi ndani ya maji kama vile baharini, ziwani, mtoni au dimbwini na mwenye mapezi na mkia ambavyo ndivyo viungo vinavyomwezesha kwenda (Akida,1981: 248). Mshairi ametumia taswira ya samaki kujadili suala la ukoloni hasa pale aliposema:

*Watu weusi na weupe  
 Mtumbwini walikuwa wamesimama, wametulia,  
 Na fimbo ndefu mikononi mwao,  
 Na macho yao wameyakazia majini.  
 Samaki ambaye, kupata hewa,  
 Aliinua kichwa chake juu ya maji  
 Utawala wa chuma ulimtoboa fuvu  
 La kichwa na kutupwa mtumbwini.  
 Halafu nilifikiria Afrika  
 Na siasa kwa ujumla  
 – Mafuvu!*  
 (Kezilahabi, 1974: 1)

Katika nukuu hapo juu tunaona jinsi mshairi alivyofanikiwa kujadili dhamira ya ukoloni akiifananisha hali ya udhaifu wa mwananchi ambaye kama akijaribu kunusa harufu ya uhuru anaadhibiwa mpaka kufa na hali ya udhaifu wa samaki ambaye kama akiinua kichwa chake juu ya maji kwa ajili ya kupata hewa anatobolewa fuvu la kichwa na kutupwa mtumbwini. Aidha, suala hili pia liliwahi kudokezwa na Ranne (2016: 158) alipohakiki kazi za mshairi huyu kwa kuelezea:

Picha ya "fuvu la kichwa" inahusiana na wanasiasa, ikionesha kuwa wao ni zana tu mikononi mwa mtu mwengine, au hajulikani. Mistari ya kwanza inaweza kuashiria hali ya ukoloni: wenyeji wa asili, samaki, ambao hawawezi kupumua kwa uhuru, hata wakiwapo nyumbani - au wakiwapo kwenye maji ya nyumbani - hali yao ni mbaya. Watu walio juu yao wanavua samaki kwa ajili ya masilahi yao tu - wakoloni Wazungu (waliofananishwa na wavuvi weupe na wasaidizi wao ni weusi) wananyonya wenyeji wa asili, (waliofananishwa na) samaki. Wavuvi wote (weusi na weupe) ni sawa, ambao labda ni watumishi weusi au wasaidizi kwa wakoloni. (Tafsiri yangu)

Kinachosisitizwa na mhakiki huyu kuititia nukuu hapo juu ni kuwa mshairi ametumia sitiari katika shairi hili ambayo ina uwezo wa kujenga picha akilini mwa msomaji akisawiri hali ya udhaifu wa mwananchi na hali ya udhalimu wa utawala. Vilevile, ameizungumzia nguvu ya utawala wakati wa ukoloni akiufananisha utawala huo na fimbo (inayotumika kupigia au kuchungia mifugo malishoni). Pia, mshairi amewafananisha wakoloni na wasaidizi wao (watu weusi na weupe) na wavuvi wanaosimama mtumbwini waliokuwa na fimbo ndefu mikononi mwao.

Kimsingi, kupitia matumizi ya taswira hii ni dhahiri kuwa Kezilahabi alitaka kufikisha ujumbe maalumu kwa wanajamii, kwamba katika wakati wa ukoloni wananchi walikuwa hawana uhuru kiasi kwamba kama mmoja wao akitaka kunusa harufu ya uhuru anaadhibiwa mpaka kufa. Taswira hii ni ya harufu/mnuso, kwani taswira hii inalenga kumfanya msomaji anuse na ahisi harufu mbaya ya mfumo wa ukoloni.

#### **4.1.2 Fisi**

Fisi ni mnyama wa mwituni mwenye ukubwa kama beberu na rangi ya kijivu na anayeaminwiwa kuwa ni mwoga na anayependa kula sana hasa mizoga. Au ni mtu mjanja (Akida, 1981: 57). Kezilahabi katika shairi lifuatalo ametumia tabia za fisi kujengea taswira zinazoakisi dhamira maalumu katika ushairi wake:

Wengine walisema ni wekundu  
Wengine walisema ni weupe  
Wengine walisema ni walafi  
Walafi kama fisi  
(Kezilahabi, 1974: 69)

Katika shairi hili mshairi amezungumzia wakoloni akiwafananisha na nzige ambao ni wadudu wenye sifa maalumu. Baadhi ya sifa hizo ni ulafi na kwa hivyo mkoloni amefananishwa na fisi (ambaye ni mnyama mlafi na mwenye tamaa). Mhakiki mwingine aliywahi kulihakiki shairi hili ni Lyimo (2009: 21) ambaye katika uhakiki wake anabainisha kwamba:

Shairi hili ni hadithi ambayo mzee/babu anaisimulia kwa watoto. Hadithi hii inahusu wavamizi waliokuja Afrika, na nzige wametumika kisitiari kama wavamizi. Walikula kila kitu ikiwa ni pamoja na utajiri wa watu. Watu hawakuwapenda hivyo, waliwafukuza. Ingawa walikimbia lakini vilibaki vizalia vyao huku Afrika.

Hivyo, mshairi anamfananisha mkoloni ambaye ni mlafi. Matumizi ya fisi katika shairi hili yamemwezesha mtunzi kujenga taswira za kiubaguzi au utenganishaji. Kutokana na matumizi hayo, msanii ameelezea picha akilini mwa msomaji ambayo inatumia kama msingi wa kuwabagua wakoloni. Katika shairi lingine Kezilahabi ameonesha kwamba ulafi wa viongozi ambao wanajifikiria wenyewe tu umefikia kiwango kikubwa sana:

Ng'ombe amekamuliwa na Wazungu (Kezilahabi, 2008:7)

Kwa mujibu wa Wamitila (Kezilahabi, 2008), Kezilahabi amefananisha nchi za Afrika na ng'ombe aliyekamuliwa na viongozi ambao wanajifikiria wao wenyewe. Kisha akaonesha kwamba tayari maziwa ya ng'ombe yamekwisha na sasa anatoa damu. Taswira hii ni ya kiishara, kwani kusawiriwa kwa damu katika hali hii ya ng'ombe ni ishara ya kufa.

#### **4.2 Dhamira ya Udhanaishi**

Mbali na kujadili suala la ukoloni, mshairi pia ametumia taswira mbalimbali za wanyama kujadili dhamira inayohusu maana ya maisha, yaani udhanaishi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), udhanaishi ni dhana inayotumiwa kuelezea falsafa ya kuwako au maisha. Kwa ujumla, uchambuzi wetu umedhihirisha kuwa Kezilahabi ameeleza mtazamo wake kuhusu maisha katika mashairi yake akitumia taswira za wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi na chui.

##### **4.2.1 Ng'ombe**

Ng'ombe ni mnyama anayetoa maziwa na kuliwa na binadamu, au ni mtu mjinga; mpumbavu (Bakhressa, 1992: 286). Mshairi ametumia taswira ya ng'ombe kuelezea fikra zake kuhusu maana ya maisha na kuwapo kwa kusema:

*Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka  
Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa.  
(Kezilahabi, 1974: 13)*

Inaonekana kuwa mshairi alipotunga shairi hilo alikuwa katika ujana wake na inafahamika kwamba kijana katika kipindi hiki labda ni mpumbavu. Kwa hivyo, mshairi alipotaka kueleza maana ya maisha akajifananisha na ng'ombe aliyefungwa na aliyefuata kamba, akiashiria mpumbavu aliyefungwa na aliyezunguka katika maisha kutokana na ugumu wake. Kuhusu shairi hilo Topan (1974: 176-179) ameeleza:

Shairi hilo linaonesha mawazo ya mwanafunzi mdogo katika kipindi muhimu cha maisha yake. Maisha hayajawahi kuwa wema, ukatili wake umesababisha kufikiria kujua.  
(Tafsiri yangu)

Vilevile, Senkoro (2011: 45,46) amebainisha:

Shairi hili limetumia taswira ya mviringo kuonyesha vile ambavyo maisha ni mzunguko usio mwisho... Taswira hii basi ndiyo kiwakilisho cha maana ya maisha kama ayaonavyo Euphrase Kezilahabi.

Kwa hivyo, maoni ya wahakiki wote wawili ambao mawazo yao yamedondolewa hivi punde yanasisitiza kuwa mshairi anaifananisha hali ya

ugumu wa maisha na hali ya ng'ombe anayezunguka akifuatilia kamba mpaka kamba hupunguzwa urefu wake hadi hatimaye hujikuta kabanwa katika kisiki kilichofungiwa kamba hiyo – na hata hutokea kamba hiyo ikamnyonga.

Dhamira ya maana ya maisha pia inajitokeza katika shairi lingine ambapo mshairi anasema:

*Ninaona kizunguzungu*

*Ninapiga kelele kama*

*Ng'ombe machinjioni*

(Kezilahabi, 1974: 23).

Nukuu hapo juu inaonyesha taswira ya ng'ombe akiwa machinjoni, na kwamba anapokuwa katika hali hiyo yumpumbavu, anazungukazunguka kama aliyefungwa na anafuata kamba tu. Wazo hili linadokeza dhamira ya udhanaishi kwa kuwa kitendo cha kuzunguka katika kamba kinaonesha kukata tamaa kwa mwanadamu sawa na ambavyo mnyama anavyojizungusha kwenye kamba akisubiri kuchinjwa anakuwa amekata tamaa. Aina hii ya taswira ni ya mwendo au mviringo.

#### 4.2.2 Mbuzi

Mbuzi ni mnyama wa kufugwa anayeliwa (Bakhressa, 1992:216). Mbali na ng'ombe, mtunzi pia ametumia mbuzi kuelezea hali ya kukata tamaa na kukosa uhuru katika maisha:

*Nami kama mbuzi nimefungwa*

*Kweney mti wa utu. Kamba ni fupi*

*Na nimekwishachora duara*

(Kezilahabi, 1974: 36)

Katika shairi hili mshairi ameifananisha hali yake ya kukosa uhuru na mbuzi aliyefungwa kwenye mti, tena kamba yenyewe ni fupi. Kwa hivyo, kama ambavyo kamba ni fupi, ndivyo maisha yanavyochukuliwa kuwa ni mafupi. Kwani wakati wowote kamba hiyo itazunguka shingoni haraka na itasababisha kujinyonga. Imebainika kwa uwazi kwamba mwelekeo wa kidhanaishi unajitokeza katika maana ya ubeti huo. Aina ya taswira hapa ni ya mwendo au mviringo. Senkoro (1995:64) anabainisha kwamba tukiangalia ubeti huu, tutaona kuwa kuna umviringo, na haya ndiyo maisha. Vilevile, kufuatia maoni ya Senkoro (1995: 64) Kezilahabi ameathiriwa (katika ubeti wake huu na kazi zake zote) na falsafa ya Kiafrika inayoyaona maisha katika mzunguko ambao

kwao jana na leo huunganishwa, na kesho kwa hakika haipo, kwani mara iwasilipo hubadilika na kuwa leo iliyojengwa katika misingi ya jana.

#### **4.2.3 Chui**

Chui ni mnyama wa msituni jamii ya paka mkubwa na mkali mwenye madoadoa meusi na manjano (BAKIZA, 2010: 56). Kezilahabi ametumia taswira ya chui kusawiri dhamira ihusuyo maana ya maisha kama inavyojitokeza hapa chini:

*Mbele chui mweusi, nyuma mwanga  
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu vyda dhambi  
Kisu, ni maisha kafiri haya  
Kama kutazama nyuma au mbele  
Ni kufa moyo mzima* (Kezilahabi, 1974: 13).

Katika shairi hili kama walivyoonesha Wafula na Njogu (2007: 75), mambo matatu yanajitokeza: (i) mshairi hajui anakokwenda wala anakotoka, (ii) hatari nyingi zimemzunguka, na (iii) kuna azimio la kujiamulia anavyotaka. Kwa ujumla, ubeti huu unazungumzia mtu aliyekata tamaa. Jazanda ya “chui mweusi” imetumiwa kuashiria giza na hatari ambayo iko karibu kumpata mtunzi. Ufafanuzi kuhusu jazanda ya chui unatufanya tuelewe kwamba chui ni mnyama wa hatari sana. Kwa hivyo, chui ni ishara ya hatari. Mshairi anasema kwamba siku zake zijazo zinaelekeea kusakamwa na mambo ya hatari sana, na kwamba hatari hiyo inawiana na hatari aliyonayo chui. Kutokana na mwelekeo huu wa kidhanaishi tunaweza kusema kwamba taswira hii ni ya kiishara kwani mshairi ametumia “chui mweusi” akiashiria hatari.

#### **4.3 Dhamira ya Ufisadi**

Ufisadi ni utumiaji mbaya wa mali ya chama, shirika au serikali, tabia ya ubadhirusi; ni utoaji na upokeaji wa hongo (Mdee na wengine, 2011: 522). Kezilahabi amejadili masuala mengi yanayohusiana na ufisadi katika mashairi yake akitumia taswira za wanyama kama vile jibwa na fahali.

##### **4.3.1 Jibwa**

Jibwa ni mbwa mkubwa, naye ni mnyama anayebweka (Bakhressa, 1992: 216). Kezilahabi ameitumia taswira ya jibwa akisema:

*Jibwa likitoka jikoni  
Ulimi lajilamba  
Piga limekariba piga  
Jibwa likishika hatamu  
Haliwezi kuacha utamu*  
(Kezilahabi, 2008:5)

Taswira ya jibwa katika shairi hilo inaashiria viongozi na wanasiasa wanaojifikiria wao wenyewe tu kwa hivyo ni rahisi kufanya ufisadi, na kama alivyosema Hassan (2013: 55) kwamba “Jibwa” ni neno lililotumiwa kiurejeleza kuwahuusu baadhi ya viongozi na wanasiasa ambao hawajali wananchi wao bali matumbo yao na yale ya familia zao” ni dhahiri kuwa jibwa ni mbwa aliyepita mipaka ya udokozi na kufikia hatua ya kuwa si mwizi tu bali jambazi wa kuogopewa na watu.

Vilevile, Drury (2015: xvi) amesisitizia maana ileile akieleza kuwa jibwa katika shairi hilo siyo jibwa halisi, bali ni kitu kingine badala yake kama ilivyoashiriwa na shairi hilo, ambapo Kezilahabi ameeleza jibwa kuwa “liloshiba hatamu”. Kimsingi, istilahi hii inatumika mara nyingi kwa maana ya uongozi (mkuu) wa chama fulani cha siasa. Hivyo, Kezilahabi ametumia taswira ya jibwa akiashiria kiongozi au mwanasiasa mwizi anayefikiria masilahi yake na manufaa ya familia yake tu, na anaweza kusababisha ufisadi mwangi katika taifa. Taswira hii ni ya kiishara, kwani mshairi ametumia “Jibwa” akiashiria kiongozi au mwanasiasa fisadi.

#### **4.3.2 Fahali**

Kwa mujibu wa TUKI (2013:106) fahali ni ng’ombe dume, dume la wanyama, au ni mtu shujaa, hodari, mwenye nguvu. Kezilahabi ameitumia taswira ya fahali kujadili ufisadi, kwa mfano, anasema ‘*Mafahali wenze matumbo wanapigana*’ (Kezilahabi, 1974: 5). Taswira hiyo inaashiria watu wenye madaraka wanaogombana kwa ajili ya madaraka hayo, na kutokana na hali hiyo wanaweza kusababisha ufisadi mwangi katika jamii yao. Mulokozi anasisitizia maana hiyo katika utangulizi wake (Aiello e Gaudioso, 2017: 24) alipoeleza kuwa siasa hizi za migongano iliyojiteze baada ya uhuru zinakejeliwa pia katika shairi la “Mafahali Wapigana”. Kauli yake “*wenze matumbo*” ni kejeli kwa kuwa ingawa watu hawa wamefaidika sana kutokana na madaraka yao hadi matumbo yao yamejaa, lakini hawajashiba na bado wanagombana kwa ajili ya kupata madaraka zaidi. Pia, Maitaria (2012: 101) anabainisha kwamba shairi hilo la ‘*Mafahali Wapigana*’ ni mionganoni mwa tungo zinazozingatia mwangwi wa methali katika utunzi na uwasilishaji kwa kuwa taswira hii inafanana na methali ya Kiswahili isemayo: *Fahali wawili hawakai zizi moja*. King’ei na Ndalu (2009: 65) wanasema kuwa methali hii hutumiwa kuelezea kwa nini viongozi wawili wawe wanagombania uongozi. Kila mmoja hujiona bora kuliko mwenzake. Taswira hii aina yake ni ya

kiishara, kwani mshairi ametumia fahali akiashiria watu wenye madaraka na wasiopatana.

#### **4.4 Dhamira ya Ujamaa**

Ujamaa ni dhana inayotumiwa kuelezea mfumo wa kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi ambao huhushisha na Rais Julius Kambarage Nyerere (Wamitila, 2003: 281). Dhamira ya ujamaa ni muhimu katika mashairi ya Kezilahabi. Katika kudadisi masuala kadhaa ya mfumo wa ujamaa, mshairi ametumia mbinu ya taswira za wanyama kama vile nyumbu, sungura na mbweha kama ifuatayo.

##### **4.4.1 Nyumbu**

Nyumbu ni mnyama wa mwituni anayefanana na farasi mwenye kimo kidogo (BAKIZA, 2010: 313). Kezilahabi ametoa wito kwa walimu waliostaafu wawe na umoja ambao kimsingi umoja ni nguzo imara ya ujenzi wa mfumo wa ujamaa:

Sikilizeni kwa makini  
Umoja hatuna:  
Twasambaratika kama nyumbu  
Tulichonacho ni woga,  
Na kinachotuangusha ni unafiki (Kezilahabi, 2008: 2).

Mshairi amefananisha kusambaratika kwa walimu waliostaafu na hali ya nyumbu waliosambaratika mwituni kutokana na woga, akidharau tabia hiyo ili waalimu wawe na umoja kufuatana na wito wa ujamaa. Kama Frans (2007: 127) alivyoeleza kuwa wito wa ‘umoja ni nguvu’ ulikuwa nguzo ya ujamaa. Mshairi ametoa wito huu kwa sababu yeye alikuwa na hamu kubwa kuwa walimu wawe na umoja. Yeye alikuwa mmoja wao baada ya kumaliza masomo yake katika Chuo Kikuu - kama alivyobainisha Topan (Kezilahabi, 1974) ambapo kuwa mwalimu katika shule kadhaa Tanzania kabla ya kujunga na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aina hii ya taswira ni ya mwendo kwani mshairi ametumia mwendo wa kusambaratika kwa nyumbu ili kusawiri hali ya walimu wasio na umoja.

##### **4.4.2 Sungura na Mbweha**

Sungura ni mnyama mdogo kama paka mwenye miguu mirefu ya nyuma, mkia mfupi na masikio marefu, huchimbua mashimo ardhini, hula majani na huenda kwa kurukaruka (BAKIZA, 2010: 379). Pia imeelezwa kuwa mbweha au bweha ni mnyama kama mbwamwitu anayekamata sana kuku (BAKIZA, 2010: 38). Kwa ujumla, Kezilahabi amewatumia wanyama hawa kujenga taswira za mfumo wa Ujamaa kwa kusema:

*Lakini kitu kimoja niliogopa daima.  
 Kuna watu wenyе viganja vikubwa zaidi.  
 Vile vile wapo wamezaо upesi upesi.  
 Kwa kuwa mimi kinywa changu kizito  
 Na viganja vyangu vidogo. Mwishowe nilisema.  
 Hao hao walinitazama kwa hasira  
 Nami bila hofu nikawatazama.  
 Tukatazamana.  
 Sungura na mbweha.  
 (Kezilahabi, 1974: 66).*

Shairi hilo linaashiria hali ya wananchi mwanzoni mwa kujitokeza kwa mfumo wa ujamaa. Maana hii inasisitizwa katika beti mbili zilizotangulia ubeti huo:

*Baba akaongeza unga wa Ujamaa ...  
 Kitu kama muujiza kikaanza kutokea  
 Baada ya mda mfupi akatoa  
 Kitu kimoja kiitwacho ugali.  
 Akaleta mboga tuliyolima sisi wenyewe.  
 Tukazunguka kula pamoja.  
 (Kezilahabi, 1974: 66).*

Kezilahabi aliposema “Baba” amekusudia Nyerere aliyeitwa “Baba wa Taifa”. Pia, aliposema “Unga wa Ujamaa” na “Ugali” ameashiria mfumo wa Ujamaa unaohusishwa na Rais Nyerere kama alivyobainisha Ranne (2016: 163,164). Kuhusu “Sungura na Mbweha” katika ubeti uliotangulia hapo juu, Kezilahabi ameifananisha hali yake ya upinzani na mfumo wa Ujamaa mwanzoni mwa kujitokeza kwake, alipokuwa akipambana na wanaouna mkono mfumo huu bila ya hofu kama hali ya Sungura anapopambana na Mbweha bila ya woga. Aina hii ya taswira ni ya kiishara, kwani mshairi ametumia hali ya Sungura anapopambana na Mbweha akiashiria hali ya wanaopinga mfumo wa Ujamaa wanapopambana na wanaouna mkono mfumo huo.

## 5.0 Hitimisho

Kezilahabi ametumia wanyama mbalimbali kujenga taswira zinazohusu masuala ya kijamii. Lengo hasa lilikuwa kufikisha ujumbe maalumu kwa msomaji. Amezungumzia dhamira ya ukoloni kwa kutumia taswira ya samaki. Samaki hao wanaashiria wananchi wasioweza kupumua, na pia wanaashiria harufu ya uhuru. Pia, ametumia fisi kujenga ishara ya mkoloni au kiongozi mlafi. Kadhalika, amejadili maana ya maisha kwa kutumia falsafa ya

kiudhanaishi. Katika kutekeleza jukumu hili ametumia taswira ya ng'ombe na mbuzi wanaowakilisha watu waliofungwa katika maisha kutokana na ugumu wake, na chui ambaye ni ishara ya hatari. Vilevile, amejadili masuala ya ujisadi kwa kutumia taswira ya jibwa ambayo ni ishara ya viongozi wanaofanya ujisadi, na mafahali wanaoashiria viongozi wanaogombania utawala. Kadhalika, amejadili dhamira ya ujamaa kwa kutumia taswira ya nyumbu wanaosambaratika mwituni kutokana na kukosa umoja na hatimaye kujenga ishara ya walimu ambao hawana umoja, na sungura anayeashiria mpinzani wa mfumo wa ujamaa, na mbweha ambaye ni ishara ya wanaouna mkono mfumo huu.

### **Marejeleo**

- Akida, H. Alidina, M. Abdala, A. Massamba, D, na Mganga, Y. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University press.
- Aiello, F. na Gaudioso, R. (2017). *Ushairi na Uhuru, Mkusanyo wa tungo za Abdilatif Abdalla na Euphrase Kezilahabi*. Napoli: Università degli studi di Napoli “L’Orientale”.
- BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (Toleo la Kwanza). Nairobi: Oxfrod University Press.
- Drury, A. (2015). *Stray Truths, Selected poems of Euphrase Kezilahabi*. Michigan: Michigan State University Press.
- Hassan, A. (2013). Kuchunguza Vipengele vya Fani katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganishi na Ulinganuzi wa Mashairi ye Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji. Tanzania: Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational House.
- \_\_\_\_\_. (1988). *Karibu Ndani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- \_\_\_\_\_. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.
- King'ei, K. na Ndalu, A. (2009). *Kamusi ya Mithali* (Toleo Jipy). Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Lyimo, E. (2009). “Matumizi ya Takriri ya Kimsamiati katika Ushairi wa Kiswahili”. Katika *Kioo cha Lughha*, Juz. Na. 7: 17-31.
- Maitaria, J.N. (2012). “Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili kwa Kutumia Kigezo cha Methali”. Katika *Mulika*, Juz. Na. 31: 89-104.
- Mazrui, A.M. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Mdee, J. Nyogu. K. na Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi. Longhorn Publisher Ltd.
- Mnyampala, M. (2014). *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: TUKI.

- Msokile, M. (1993). *Msingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational publishers Ltd.
- Ranne, K. (2016). “The Image of Water in the Poetry of Euphrase Kezilahabi”. Katika *The Finnish Oriental Society*. Juz. 118.
- Saleh, A. (1990). “Mtindo wa Mashairi Huru: Maoni na uandishi”. Katika *Jarida la Lughha*. Juz. Na. 4: 84–93.
- Senkoro, F.E.M.K. (1995). “E. Kezilahabi: Shaaban Robert wa Pili”. Katika *Kioo cha Lughha*, Juz. Na. 1 (1): 61-69
- \_\_\_\_\_. (2011). *Fasihi*, Dar es Salaam: KAUTTU.
- \_\_\_\_\_. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Topan, F. (1974). “Modern Swahili Poetry”. London: Katika *Bulletin of the School of Oriental and African Studies, University of London*, Juz. Na. 37 (1).
- TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press
- Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K.W. (1998). “A Philosophical Labyrinth: Tacing Two Crtcial Motifs in Kezilahabi’s Prose Works”. Katika *Kiswahili*. Juz. Na. 55: 79-91.
- \_\_\_\_\_. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- \_\_\_\_\_. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.